

Rafiki Yangu Yesu Kristo (My Friend Jesus Christ)

Na

John Kombo

Rafiki Yangu Yesu Kristo (My Friend Jesus Christ)

Na

John Kombo

June 14, 2013

Rafiki Yangu Yesu Kristo

Yesu aliwaambia wanafunzi wake maneno hayo, “*Ninyi mmekuwa rafiki zangu mkitenda niwaamruyo. Siwaiti tena watumwa; kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu.*” (Yohana 15:14-15).

Kulingana na maneno ya Yesu, tunaweza kusema kwamba mtu anakuwa na sifa za kuwa rafiki wa Yesu kama ni mtiifu kwa kile anachokisema Yesu. Hivyobasi, maneno ya Yesu ya upendo yaliendelezwa kwa wale waliotii amri zake. (Yohana 14:15, 21; Mdo. 10:42; 1 Yoh. 3:23-24). Bwana wetu Yesu Kristo amekuwa na wanafunzi lakini hakuwahi kuwaita “rafiki zangu” mara nyingi aliwaita “wanafunzi wangu”. Kwa nini aliwaita “rafiki zangu?” Aliwafundisha mambo yote aliyosikia kutoka kwa Baba yake; walitii? Ndiyo, walitii, na hii ikawapa sifa ya kuitwa rafiki. Aliwaamini pasipo kuwa na shaka kwamba chochote walichosikia kutoka kwake wangefundisha wengine pia. Alimaliza kazi yake lakini alichokiitaji ni kuwa na watu aliowaamini kufanya kazi kama akirudi kwa Baba yake. Hapa kuna watu ambao Yesu aliamini akawaita “rafiki” Je nasi ni “rafiki” wa Yesu? Au nyie ni wanafunzi wake tu lakini siyo rafiki. Hata Yuda Iskariote alikuwa mwanafunzi wake lakini alimsaliti. (Marko 14:43-52; Luka 22:47-53; Yohana 18:2-12). Tuna ndugu, lakini wote sio rafiki zake. Kuwa makini!

Mtume Paulo aliandika waraka wa Wafilipi wakati alipokuwa gerezani Rumi kati ya karne ya AD 61-63: sura ya 3, msitari wa 1, Paulo aliandika, “...*hatimaye ndugu zangu furahini katika Bwana ...*” katika sura ya 4, msitari wa 4, Paulo akarudia tena, “...*furahini katika Bwana siku zote. Tena nasema furahini!*”

Hata kama Paulo alikuwa gerezani, alikuwa na furaha na mwenye ujasiri. Alikuwa tayari kuonyesha furaha yake katika neno “*furahi*” aliwaandikia watu aliowamini na injili ya Yesu Kristo. Msisitizo wa Paulo hapa ni kufafanua uasilia wa maisha ya Mkristo. Mtu mwingine anafurahi kutokana na tukio fulani.

Mwisho, lakini ni mhimu, tunasoma katika 2 Timotheo 2:2, “*Mambo uliyosikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaoweza kuwafundisha na wengine pia.*”

Ilikuwa ni wajibu wa Timotheo kuwaangalia watu waaminifu naa kuwapa maagizo ili kubeba ukoo huu wa kiroho. Mtu mwaminifu ni yule anaetazama kwamba kazi aliyopewa imeisha. Huwezi kuwa mwaminifu kwa Mungu pasipo kuwa mwaminifu katika kazi yake. Huwezi kuwa mwaminifu katika kazi yake wakati huwezi kuimaliza kazi hiyo, ili uweze

kunena kama Paulo, “*Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda,*” (2 Tim. 4:7).

Mungu awatie nguvu, afungue milango, na kuwapa hekima watumishi wake Kenya, Tanzania, na Uganda, na sehemu zote za dunia. “*Makanisa yote ya Kristo yawasalimu.*” (Rum. 16:16).

John Kombo Nandwa
Kanisa la Kristo Barut
Nakuru, Kenya

